Je, stima, gesi na maji ilikatwa? Ninaweza kuzirudisha vipi?

Ofisa wa moto anayesimamia anaweza kuwa alihitaji kukata stima, maji au gesi kwa sababu ya usalama wakati wa moto.

Kama una bima,kampuni ya bima yako wanaweza kupanga huduma hizi kurudishwa tena. kama hauna bima, utahitaji kupanga mwenyewe kwa kupiga simu kwa kila mmoja wanaotoa huduma au wanabiashara wa kazi ya mkono.

Wanaokupa huduma ya stima, maji na gesi kwako watatuma mtu wa kazi ambaye amehitimu kukagua na kurekebisha uharibifu yeyote katika huduma yako, na kupanga kuzirudisha.

Ni kwa nini waandishi wa habari wako hapa?

Waandishi wa habari mara kwa mara wanaripoti kuhusu moto kwenye tangazo ya habari. Kama mwandishi wa habari amekukukaribia kwa mahojiano. Unaweza kuamua kama unataka kuzungumza nao au la. Kama umekubali kuhojiwa, unaweza kujadiliana nao kabla ya mahojiano kuhusu aina ya maswali ambazo watakuuliza ili uweze kujua ni nini utatarajia. Unaweza kuuliza ofisa wa kuzima moto kukusaida au kuwa kama mwakilishi.

Kama unahisi hauna raha kuhusu sehemu yeyote ya mahojiano, mweleza mwandishi wa habari kuwa haupendi kuendelea. Kama sababu ya moto haijanguduliwa na bado inapelelezwa, ni bora kutojadiliana jambo lolote na waandishi wa habari.

Ninahitaji kuzungumza na mtu, ni wapi ninaweza kwenda?

Moto ya nyumba ni tukio ya kutatanisha ambayo inaweza kuleta uchungu kwa akili na hisia, hii ni kawaida, lakini unahitaji kufikiria namna vile wewe na familia yako mtaweza kuendelea. Ni muhimu kuuliza usaidizi na kuzungumza na mtu kuhusu namna unavyoendelea kama vile familia, marafika au mshauri.

Kasisi wa FESA anaweza kutoa usaidizi kwako au familia yako. Ofisa wa moto anayesimamia anaweza kumwita kasisi kwa nyumba yako ili kukupa usaidizi kwa maono ya huzuni papo kwa hapo na kukusaidia kupanga mpango wa siku zijao. Kuna idadi ya kampuni ambazo zina laini ya simu ya usaidizi masaa zote ambazo unaweza kupiga.

Simu ya usaidizi masaa ishirini na nne:

FESA Chaplain **(08) 9485 7800**
(hii ni huduma ya pager, utahitaji kuwacha ujumbe)

Crisis Care **(08) 9223 1111**

The Samaritans **(08) 9381 5555**

Lifeline **13 11 14**

Ofisa wako anayesimamia _____

Wanatoka _____stesheni ya kuzima moto

kwa _____ zamu ya kazi

Nambari yao ya simu _____

Ofisa wako wa moto anayesimamia atakusaidia kwa kujaza sanduku ambazo mumezungumzia ambazo unahitaji sasa kufwatilia:

Kama una bima:

- ☐ Wasiliana na kampuni ya bima yako

Kampuni ya bima yako itaangalia:

- ☐ makao ya kighafula
- ☐ chakula na mavazi ya kighafula
- ☐ kuwasiliana na kampuni kusafisha uharibifu
- ☐ kupata maji,gesi na stima kuangaliwa na kurudishwa

Kampuni ya bima yako inatoa ushauri kwa:

- ☐ ni nani utawasiliana nao kwa usalama wa nyumba yako
- ☐ wakati mpimaji wa bima atakuja nyumbani mwako
- ☐ wakati wa kuwasiliana na wafanyi kazi wa mkono kurekebisha nyumba yako

Kama hauna bima au hati yako haigharamii, wasiliana:

- ☐ huduma za kutoa makao, chakula na mavazi ya kighafula
- ☐ kampuni ya kulinda usalama wa nyumba yako
- ☐ mawakili wa kutoa ushauri na usaidizi (pamoja na kasisi wa FESA)
- ☐ kampuni ya kusafisha uharibifu
- ☐ fundi wa stima kurekebisha uharibifu na kurudisha stima
- ☐ fundi wa bomba kurekebisha na kurudisha maji na gesi
- ☐ Kampuni kurekebisha nyumba yako.

OCTOBER 2010

Kujitoa lawama
Maelezo katika mwongozo hii imetolewa na Fire and Emergency Services Authority (FESA) kwa kujitolea kama huduma ya umma. Mwongozo hii imetayarishwa kwa imani nzuri na imetolewa mahala ambayo inaaminiwa kuwa inatumainiwa na ni sahihi kwa wakati wa chapisho. Hata hivyo, kutumainiwa na usahihi wa maelezo haiwezi kudhaminiwa na FESA inajitoa katika lawama ya tukio ya jambo kutokea, au kwa kitu ambayo imekoswa kufanyawa au imefanywa kwa kutegemea maelezo haya na kwa jambo litokealo kutona na au kuto tokana na tukio hii au ukosefu hii kwa ajili ya tokeo au jambo lililoachwa. Kijitabu hii imekusudia kama mwongozo pekee yake na wasomaji wanapaswa kupata mawaidha yao ya kujitawala na kujitafutia maelezo inayaohitajika.

Government of **Western Australia**
Fire & Emergency Services Authority

FESA
Fire & Emergency Services Authority of Western Australia

KUINUKA BAADA YA MKASA...

JAMBO LA KUFANYA BAADA YA MOTO NYUMBANI MWAKO

swahili

Government of **Western Australia**
Fire & Emergency Services Authority

FESA
Fire & Emergency Services Authority of Western Australia

Kama moto imeharibu au kutia hasara nyumba yako unaweza kupata mshtuko na kuwa katika hali ya kutatanisha. Inaweza pia kuwa ngumu kukubali yaliotokea. Hii ni kawaida na hisia hizi itapungua kwa wakati. Kwa muda hii kuna vitu ambavyo unaweza kufanya kukusaidia kuwa imara tena.

Kijitabu hii itakusaidia kujua hiari zako,namna ya kupata mavazi mengine na kuweza kuangalia ni wapi unaweza kwenda kuishi kama hauwezi kukaa nyumbani mwako. Ofisa wa kuzima moto anayesimamia mahala palipo na moto pia anaweza kukusaidia.

Sina mahali ya kukaa usiku hiyo. Ni nini kitanifanyikia mimi na familia yangu?

Kama nyumba yako ina bima, piga simu kwa kampuni ya bima yako kwasababu inaweza kuwa hati ya bima yako inakupa mahali pa kukaa kwa tokea la ghafula. Kuna simu ambazo unaweza kupiga baada ya masaa ya kawaida ya kazi. Kama hauna bima, kunauwezekano kukaa na familia au marafiki.

Njia mengine ni kuwasiliana na Department of Housing, na wataweza kukusaidia kupata mahala pa kukaa kwa muda mfupi wakati wa ugumu na kusaidia kupata mahala pa kukaa kwa muda mrefu, au idara ya uangalizi wa kipeo katika jamii.

Department of Housing, Homeless Advisory Service:
simu ya bila malipo 1800 065 892
(kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi na moja jioni jumatatu hadi ijumaa)

Department for Communities, Crisis Care:
(08) 9223 1111 au simu ya bila malipo 1800 199 008
(mjana au usiku)

Kampuni yangu ya bima inaweza kuhusika vipi?

Kama wewe ndiye mwenyeji wa mali utahitaji kuwaeleza kampuni ya bima yako haraka iwezekananvyo. Watatuma mwakilishi kukisia gharama ya uharibifu na kuamua kiasi ya malipo.

Kama wewe ni mpangaji wa nyumba na una bima kwa vitu yaliyomo, pamoja na kumweleza mpangisha nyumba wako kuhusu moto hii, unatakiwa pia kuwasiliana na kampuni ya bima yako.

Je, kama sina bima?

Utahitaji kupanga matengenezo ya nyumba yako lakini kumbuka kutegemea jamii na marafiki wako kukusaidia.

Kuhusu nyumba yangu, Je itakuwa salama kwa usiku hiyo?

Kama wewe ndiye mwenye mali, ni jukumu yako kupanga usalama wa nyumba yako unapongoja bima yako kupimwa. Kampuni ya bima yako watakupa mawaidha na kama mwakilishaji yuko pamoja nawe, wanaweza kupanga kampuni kulinda usalama ya nyumba yako. Kama una maswali yeyote, zungumza na polisi katika mtaa yako.

Kama kuna sehemu ambazo zimeharibika zaidi kwa ajili ya kuwachwa wazi, State Emergency Service (SES) wanaweza kuweka tarpaulins na kukaza vitu ambazo zimelegalega. Uliza ofisa wa kuzima moto anayesimamia au ofisa wa polisi kupanga hii. Au piga simu SES nambari 132 500.

Kila kitu kimepotea kwenye moto. Nitalisha na kuvisha vipi familia yangu?

Kama una bima, angalia na kampuni ya bima yako kama wanaweza kusaidia na chakula na mavazi kupitia hati ya bima yako.

Kama hauna bima au bima yako haizingatii haya, Department for Child Protection au Department for Communities Crisis Care, wanaweza kusaidia na chakula, mavazi, makao ya muda mfupi wa kighafula na mahitaji mengine ya lazima.

Department for Child Protection:
(08) 9222 2555, simu ya bila malipo 1800 622 258
(kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi na moja jioni jumatatu hadi ijumaa)

Department for Communities, Crisis Care:
(08) 9223 1111 au simu ya bila malipo 1800 199 008
(mjana au usiku)

Kasisi wa FESA pia anaweza kusaidia na kukuwezesha kuwasiliana na watu ambao wanaweza kutoa mahitaji ya lazima. Tafadhali uliza ofisa wa kuzima moto anayesimamia ili kupanga haya au unaweza kuwasiliana na kasisi kupitia pager kwa nambari (08) 94857800 na kuwaja ujumbe.

Je ninaweza kuondoa vitu vya kibnafsi?

Kama sehemu ya nyumba yako hazijaharibiwa na ofisa wa kuzima moto anayesimamia au ofisa wa wakupeleleza moto amekueleza kuwa ni salama kuingia, ungependa kuchukua vitu vifwatavyo:

- kitambulisho
- kadi zako za credit
- vitabu vyako ya benki ya cheki
- stakabadhi zako za kisheria
- maelezo ya bima
- madawa
- miwani yako ya macho
- bidhaa ya kutumia kusikia au za kibinafsi
- mapambo ya vito,kitabu cha kutilia picha, kada ya picha
- Vitu mengine ya thamana

Hata hivyo, ni bora zaidi kuangalia na kampuni ya bima yako kabla ya kuondoa kitu yeyote.

Moto imechafua nyumba yangu. Ni wakati gani ninaweza kusafisha?

Wazima moto kwa kawaida wanatumia maji iliyo na mkazo kuzima moto. Wanahakiskisha kwa kila juhudi kupunguza kiasi ya uharibifu au kulinda bidhaa za nyumba na vyombo vya nyumbani ili uweze kurudi nyumbani mwako kwa haraka.

Kama moto ilikuwa na uzito ndani ya nyumba yako, kunauwezakano utahitaji kusafisha. Angalia na ofisa wa kuzima moto anayesimamia, ofisa wa wakupeleleza moto au ofisa wa polisi ili kujua ni wakati wa kuanza kusafisha. Kama kuna upelelezi au kutathmini abayo inafanywa kunaweza kuwa na sehemu ambazo hauwezi kusafisha mwanzoni. Unahitaji kuangalia na kampuni ya bima yako kuona kama hati ya bima yako inaruhusu wafanyi biashara wa kufanya usafi.

Ni nini jukumu ya ofisa wa kupeleleza moto?

Kama ofisa wa moto anayesimamia tukio fulani hawezi kujua chanzo cha moto, wanaweza kuwaita ofisa wa kupeleleza moto. Kama kuna mtu ambaye amejeruhiwa vibaya au amefariki kutokana na moto hii polisi watahudhuria.

Ni jukumu ya ofisa wa kupeleleza moto au ofisa wa polisi kuhakikisha kuwa nyumba yako iko salama wakati upelelezi inafanyika. Wata weka ukanda kama kizuizi kuzunguka nyumba yako, ili watu wasiweza kuingia kwasababu inaweza kuwa siyo salama na pia inaweza kusumbua upelelezi.

Kama unahitaji kuingia nyumbani mwako katika hali hii ofisa wa polisi au ofisa wa kupeleleza moto anaweza kuambatana nawe. Mara watakapomaliza upelelezi wataweza kuacha utawale nyumba yako.

Ni nini jukumu ya kundi ya polisi kuhusiana na kuchoma moto kusudi?

Kundi ya polisi inayohusiana na kuchoma moto kusudi watahudhuria kama wameulizwa na ofisa wa kupeleleza moto. Wanafanya kazi kila mara kushiriakiana na huduma za kuzima moto na wataenda palipo na moto kama moto hii imedhaniwa ni enye kushuku au kwa kusudi, haitambuliki au mtu amekufa.